TANGAZO LA SERIKALI Na. 677 la tarehe 25/11/2022

SHERIA YA MIPANGOMIJI,
(SURA YA 355)

# AMRI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 8(1) na 23(1))*

AMRI YA MPANGO WA URASIMISHAJI WA ENEO LA KAREMA YA MWAKA, 2022

Jina

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Mpango wa Urasimishaji wa Eneo la Karema ya Mwaka, 2022.

Kutangazwa kwa eneo la upangaji

2. Eneo lililoainishwa katika Jedwali la Amri hii linatangazwa kuwa eneo la upangaji kwa madhumuni ya urasimishaji.

Mpango wa kina wa eneo

3. Mpango wa kina wa eneo lililoainishwa katika Jedwali unaandaliwa na kuhifadhiwa kwa Mkurugenzi wa Mipangomiji na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Tanganyika.

JEDWALI

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

Eneo la Upangaji lipo ndani ya mipaka ifuatayo:

"Unaanza kwenye alama P1 yenye majira - nukta 216061.03E, 9245322.74N iliyopo katika mwambao wa Ziwa Tanganyika karibu na bandari ya Karema; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini – Mashariki katika uelekeo N 19°02'30"E kwa kufuata barabara ya kwenda Sekondari ya Karema kwa umbali wa kilomita 0.626 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba P2 yenye majira - nukta 216273.94E, 9245911.82N; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini – Mashariki katika uelekeo wa S84°03'33"E kwa umbali wa kilometa 1.12 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba P3 yenye majira - nukta 217388.51E, 9245796.07N; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini – Mashariki katika uelekeo wa S21°25'48" kwa umbali wa kilomita 0.585 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba P4 yenye majira - nukta 217602.55E, 9245250.73N; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini – Magharibi katika uelekeo wa S35°11'42"W kwa umbali wa kilomita 0.542 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba P5 yenye majira - nukta 217289.73E, 9244807.19N; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini – Magharibi katika uelekeo wa N67°14'14"W kwa kufuata mwambao wa Ziwa Tanganyika kwa umbali wa kilomita 1.32 hadi ulipoanzia"

Dodoma,
8 Novemba, 2022

ANGELINE S. MABULA,
*Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi*